



A colorful illustration of three people on a beach. A man in the center wears a lei and holds a surfboard. A woman to his left wears a lei and sunglasses. A small child to his right also wears a lei. They are standing on a white sandy beach under a blue sky.



KUSOMA  
hutokea  
mahali popote  
wakati wowot  
na kwa kila  
mtu.



TUNAPODADISI na KUGUNDUA mengi kutuhusu sisi wenye wengine na watu wengine...

... kila wakati TUNAPOSIKILIZANA sisi kwa sisi na maisha yanayotuzunguka



The illustration depicts a variety of daily life scenes in East Africa. In the foreground, a woman in a yellow and green patterned dress is shown from the side, looking into a small handheld mirror. To her left, a man in a red shirt and grey pants carries a baby on his back, with a monkey clinging to his shoulder. In the center, a man in a white traditional robe (agaci) holds a young child. To the right, a woman in a purple and green patterned dress carries a child on her back. Above the woman in yellow, a thought bubble contains an illustration of a person lying in a hospital bed. The background features a light blue gradient with a faint map of Africa inside a large white circle. Diagonal text in Swahili is overlaid on the upper right side of the image.

# Kusomea nyumbani

## Je, bango hili linamlenga nani?

- Ni la aina zote za watoto wenyewe ulemavu na wale wasio na ulemavu.
- Ni la **kila mtu**- akina baba na akina mama, walezi, watoto, vijana, ndugu, babu na bibi, wajomba na shangazi...

## Bango hili linahusu nini?

Maisha huweza kuwa magumu wakati shule zinapokuwa zimefungwa na watoto wakiwa nyumbani. Watu wazima wanataka kuwasaidia watoto na vijana kusoma kama wafanyavyo wakiwa shulenii lakini siyo rahisi.

Bango hili linaonesha njia nyingi ambazo tayari familia zinifuata kufanikisha kusomea nyumbani. Mtu yeyote anaweza kutumia maoni na ubunifu wake binafsi kuendeleza mbinu hizi za ujifunzaji.

## Kwa nini bango hili lilitengenezwa?

Bango linasaidia familia kutambua zaidi namna kusoma kunavyotoka nyumbani na jinsi **kusomea nyumbani** kunavyoweza kuboresha kusoma katika shule na katika jamii.

## Jinsi ya kutumia bango hili?

- Tundika bango ukutani kwako linakoweza kutazamwa na kila mtu nyumbani. Waombe watoto ili wakusaidie kuamua mahali pa kulinikisha bango hilo.
- Angalia kwenye bango wakati wowote.
- Fikiria juu ya picha. Ni picha gani ambazo unapenda kuangalia sana?
- Je, unaona nini? Unafikiri ni nini kinatendeka katika picha hizi?
- Je, picha hii inakupa mawazo gani ya kusomea nyumbani?
- Hakuna majibu yasiyo sahihi au yaliyo sahihi.

# Mambo ya kukumbuka unaposomea nyumbani

## Kusoma hutokea kila wakati **TUNAPOSIKILIZANA** sisi kwa sisi na maisha yanayotuzunguka...

- Kusikiliza kunatoka baina ya kila mtu. Watu wazima huwasikiliza watoto, watoto huwasikiliza watu wazima vile vile na watoto huwasikiliza watoto wenzao.
- Omba usaidizi ikiwa huelewi kitu fulani. Mtu yeyote anaweza akusaidia.
- Simulia hadithi kwa kutumia ishara ya mikono au kichwa na ishara uso. Hakikisha kuwa kila mtu anaweza kukuona unaposimulia hadithi.
- Yasikilize mazingira yanayokuzunguka - ndege, wanyama, mvua. Jaribu kuziigiza sauti hizo.

## Kusoma hutokea kila wakati **TUNAPOCHEZA** na **KUFURAHIA** kuwa peke yetu au na mtu mwengine...

- Kila siku, zunguka zunguka kwa njia yoyote uwezavyo. Cheza. Ruka. Zunguka, Bingirika.
- Fanya mabadiliko kwa michezo ili kila mtu aweze kuijiunga. Hii inaweza kuwa kubadilisha sheria au mienendo.
- Anzisha michezo mipyka kisha uwafuze wengine namna ya kuicheza michezo hiyo.
- Ukiwa pekee yako, unaweza kuwa kimya au kuwa na shughuli nyingi kulingana na jinsi unavyohisi wewe.

## Kusoma hutokea kila wakati **TUNAPODADISI** na **KUGUNDUA** mengu kutuhusu na kuhusu sisi kwa sisi...

- Jaribu kufanya kitu kipyaa, hata ikiwa si rahisi mwanzoni.
- Jifunzeni kutoka kwa ninyi kwa ninyi. Tafuta mtu anayeweza kukufundisha kitu fulani unachotaka kujifunza.
- Otesha mimea. Tunza mti. Rekebisha kitu. Jenga kitu. Badilisha kitu.
- Uliza maswali: Kwa nini hii inatokea? Je, hii inafanya vipi kazi? Itakuwaje nikibadilisha hii?

## Kusoma hutokea kila wakati **TUNAPOBUNI** na **KUVUNDA** kitu kwa kutumia kitu chochote kinachotuzunguka...

- Tumia vifaa vyovoyote ulivyo navyo, kama vile chupa zilizotumika tayari, paketi, vijiti, matope kufanya vitu vingi tofauti. Kitu chochote kinawenza kutumika kuwasaidia kusoma.
- Tumia ubunifu wako pamoja na vifaa upatavyo kutunga hadithi. Hadithi hizi zinaweza kuwa za kweli/halisi au za kubuni.
- Igiza hadithi zako ulizobuni. Waambie watu wengine kile ulichokibuni. Simulia hadithi!
- Kata herufi kutoka kwa pakiti za zamani na utengeneze maneno.

## Kusoma hutokea kila wakati tunapojihisi kuwa **SALAMA** na **KUPENDWA** hata tunapokabiliwa na shida...

- Kujihisi salama na kupendwa ni msingi wa kusoma na kukua. Bila kujihisi salama na kupendwa inaweza kuwa ngumu sana kwa mtu yeyote kusoma.
- Mjaliane na kusaidiana nyinyi kwa nyinyi. Mhurumiane, haswa wakati wa nyakati mgumu.
- Kujali hufanyika kati ya kila mtu. Watu wazima huwajali watoto, watoto huwajali watu wazima, watu wazima hujali watu wazima na watoto huwajali watoto.
- Kila mtu hujifunza na kuiga tabia za watu wanaomzunguka. Onyesha tabia unayotaka kuona.